**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA**

**MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI**

**711** **KISWAHILI**

**Muda: Masaa 3** **Ijumaa, 06th May 2011 Asubuhi**

**Instructions.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali kumi na sit (16).
2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A na maswali mawili kutoka kila sehem **B** na **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** Zina jumla ya alama **sitini (60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha majibu.

maktaba.tetea.org
TETEA



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali yote kutoka sehemu hii. Kila swali lina alama 4.

1. (a) Eleza maana ya nomino za dhahania.

   (b) Taja nomino mbili za dhahania na tunga sentensi moja kwa kutumia mojawapo.

2. (a) Fafanua maana ya kishazi huru.

   (b) Toa mfano mmoja wa kishazi huru katika sentensi na ukieleze.

3. Eleza maana ya ngeli ya KI-VI na taja sifa tatu za majina yanayopatikana katika ngeli hiyo.

4. Eleza maana ya upatanisho wa kisarufi na toa mifano miwili ya sentensi zinazofuata kanuni hiyo.

5. Toa maana ya kauli ya utendewa na tunga sentensi moja inayoonyesha matumizi ya kauli hiyo.

6. Eleza tofauti kati ya vielezi vya namna na vielezi vya mahali kwa kutoa maana na mifano miwili ya kila aina.

7. Tofautisha kati ya viwakilishi vya nafsi ya pili umoja na viwakilishi vya nafsi ya pili wingi kwa kutoa maana na mifano.

8. Eleza maana ya methali na toa mifano miwili ya methali zinazohimiza mshikamano wa kijamii.

9. (a) Taja vipengele viwili vya fani vinavyopatikana katika riwaya.

   (b) Eleza umuhimu wa kila kipengele ulichotaja.

10. Toa maana ya istilahi zifuatazo katika fasihi simulizi:

    (a) Hadithi-fupi

    (b) Wahusika

    (c) Kichwa cha hadithi

    (d) Mtindo



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali mawili kutoka sehemu hii. Kila swali lina alama 15.

**Soma kifungu kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata:**

Katika miaka ya hivi karibuni, matumizi ya lugha ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali yameongezeka kwa kiwango kikubwa. Serikali imekuwa ikihimiza matumizi ya Kiswahili katika sekta za elimu, mahakama, utangazaji na hata katika siasa. Viongozi wengi sasa hutumia Kiswahili katika hotuba zao, jambo ambalo linaweka lugha hiyo katika nafasi ya heshima na mamlaka. Vilevile, taasisi za elimu za juu zimeanza kufundisha baadhi ya kozi kwa Kiswahili, hali inayotoa fursa kwa wanafunzi wengi kuelewa vizuri yaliyofundishwa.

Hata hivyo, licha ya mafanikio haya, bado kuna changamoto kadhaa. Baadhi ya watu hudhani kuwa Kiswahili ni lugha ya watu wasioelimika na hivyo hukipa kisogo. Aidha, baadhi ya fasihi na istilahi za kitaaluma bado hazijatafsiriwa kwa Kiswahili kwa ukamilifu, hali inayowapa walimu na wataalamu kazi ya ziada. Licha ya hayo, juhudi za wataalamu wa Kiswahili kuendeleza istilahi na fasihi ya taaluma zinapaswa kupongezwa. Kwa ujumla, ni wazi kuwa Kiswahili kina nafasi muhimu katika maendeleo ya taifa, lakini mafanikio yake yatategemea juhudi za pamoja kutoka kwa serikali, wataalamu na jamii kwa ujumla.

11. (a) Eleza maudhui matatu yaliyopo kwenye kifungu.
    (b) Taja changamoto mbili zinazokwamisha maendeleo ya Kiswahili kama zilivyotajwa.
    (c) Eleza umuhimu wowote wa Kiswahili kwa maendeleo ya taifa kama ulivyojitokeza.

12. Kwa hoja sita, eleza jinsi shule za sekondari zinavyoweza kukuza matumizi ya Kiswahili kwa wanafunzi wa viwango vyote.

13. Tunga mazungumzo mafupi baina ya mwanafunzi na mwalimu wake kuhusu umuhimu wa kutumia Kiswahili sanifu katika mawasiliano ya kila siku.

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali mawili kutoka sehemu hii. Kila swali lina alama 15.

14. Kwa hoja sita, eleza jinsi mashairi ya Kiswahili yanavyotumika kueleza hali za maisha ya jamii za Kiafrika.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

15. Tathmini nafasi ya wahusika wa kike katika riwaya unazozisoma. Taja riwaya angalau mbili na eleza kwa mifano.

16. Eleza kwa hoja sita jinsi lugha ya Kiswahili inavyoweza kuchangia katika utatuzi wa migogoro ya kijamii na kisiasa nchini Tanzania.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org